**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO**

# BARAZA LA MICHEZO LA TAIFA (BMT)

**21 Januari, 2026**

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## UCHAGUZI WA SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA (TBF)

Baraza la Michezo la Taifa (BMT) linapenda kuwataarifu wanachama na wadau wa mchezo wa mpira wa kikapu Tanzania, kuwa Uchaguzi wa Viongozi wa Shirikisho la mpira wa kikapu Tanzania (TBF) unatarajiwa kufanyika tarehe 28 Februari, 2026, Jijini Dodoma.

Fomu za kugombea nafasi tofauti katika uchaguzi huo zitaanza kutolewa katika Ofisi za BMT zilizopo Uwanja wa Benjamin Mkapa tarehe 22 Januari, 2026 hadi Februari 10, 2026 na zinapatikana katika tovuti ya Baraza ambayo ni www.bmt.go.tz

Aidha, Usaili wa wagombea wa nafasi hizo unatarajiwa kufanyika tarehe 27 Februari, 2026 Jijini Dodoma.

Nafasi zinazogombewa katika uchaguzi huo ni pamoja na:

| Nafasi | Ada |
|---|---|
| 1. Rais<br>2. Makamu wa Rais | 600,000/= |
| 3. Katibu Mkuu<br>4. Katibu Mkuu Msaidizi | 500,000/= |

**Sifa za wagombea**

- **i.** Awe Raia wa Tanzania
- **ii.** Awe na Elimu angalau ya Kidato cha Nne
- **iii.** Awe na uzoefu juu ya nafasi ya Uongozi anayogombea.
- **iv.** Awe na ufahamu wa juu ya Shirikisho na Taasisi zake, ajue shughuli zake na uendeshaji.
- **v.** Awe na uwezo wa kuzungumza na kuandika lugha ya Kiswahili na kiingereza.
- **vi.** Awe na umri usiopungua miaka ishirini na tano (25), isipokuwa wale wanaogombea nafasi ya Rais na Makamu wa Rais ambao wanatakiwa wawe na umri usiopungua miaka 30.

vii. Awe hajapatikana na hatia ya kosa lolote la jinai hususani linalogusa na kushusha hadhi, utu na haiba mbele ya jamii (kama ubadhirifu, wizi, mauaji, madawa ya kulevya n.k)

viii. Awe amewahi kuwa mchezaji wa mpira wa kikapu, au kuhudhuria mafunzo ya ualimu wa mpira wa kikapu, uamuzi, utawala wa michezo, tiba ya wanamichezo, au utunzaji na utengenezaji wa viwanja.

ix. Wagombea wa nafasi ya Rais na makamu wake, lazima wawe na elimu na uzoefu wa kutosha na mambo ya utawala wa michezo, hasa kuongoza mchezo wa mpira wa kikapu kwa ngazi yoyote nchini.

Malipo ya fomu yafanyike katika Akaunti ya Baraza, kwa kutumia mfumo mpya wa malipo ya Serikalini.

Ili kupata namba ya malipo (Control Number) mgombea anashauriwa kupiga namba ya simu ifuatayo; 0754 770 550

Aidha, fomu ya kugombea iwasilishwe Baraza ikiambatishwa na risiti ya malipo pamoja na nakala za nyaraka kulingana na sifa mahususi zilizoainishwa katika katiba ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania.

BMT inatoa wito kwa yeyote mwenye sifa kwa mujibu wa Katiba ya Shirikisho la Mpira wa Kikapu Tanzania (TBF) kujitokeza kuchukua fomu kwa ajili ya uchaguzi huo na maendeleo ya Mchezo huo nchini.

## RATIBA YA UCHAGUZI MKUU WA SHIRIKISHO LA MPIRA WA KIKAPU TANZANIA (TBF)

| TAREHE | TUKIO | MHUSIKA | SIKU |
|---|---|---|---|
| 21 Januari 2026 | Kutangaza kwa Umma mchakato wa uchaguzi wa TBF na nafasi zinazogombewa. | Baraza la Michezo (BMT) | **1** |
| 22 Januari – 10 Februari 2026 | Wagombea kuanza kuchukua fomu za kugombea. Mwisho wa kuchukua na kurudisha fomu za kuomba uongozi ni tarehe 10 Februari, 2025 saa 10 kamili jioni. | Wagombea Wote | **14** |
| 11 -13 Februari 2026 | Kikao cha kuchuja majina ya Wagombea na kuwajulisha Wagombea hatua za mchujo. | Kamati ya Uchaguzi | **3** |
| 14-16 Februari 2026 | Kuchapisha na kubandika kwenye mbao za matangazo orodha ya awali ya wagombea. | Kamati ya Uchaguzi | **3** |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 16-18 Februari 2026 | Kipindi cha kupokea na kuweka pingamizi kwa wagombea (Mwisho saa 10 kamili jioni). | Wagombea | **3** |
| 19-21 Februari 2026 | Kusikiliza pingamizi na kutoa matokeo ya pingamizi. | Kamati ya Uchaguzi, Mlalamikaji na Mlalamikiwa | **3** |
| 22-27 Februari 2026 | Kipindi cha Kampeni kwa Wagombea | Wagombea | **6** |
| 27 Februari 2026 | Kufanya usaili wa wagombea waliochujwa | Kamati ya Uchaguzi na Wagombea | **1** |
| 28 Februari 2026 | **UCHAGUZI MKUU WA TBF** | Wote | **1** |

**Imetolewa na**

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano**